



<p>Parent-Teacher Conferences</p> <p>For grades primary to 12, Parent-Teacher meetings occur twice a year. The dates are posted on the school calendar and communication will be sent to parents. To attend, parents must register online to book an appointment. Parents are encouraged to attend the meeting which is 10-15 minutes.</p> <p>Parent-Teacher meetings are conversations between the parent and the teacher about what is best for the child. It is an opportunity to discuss your child's progress. The teacher will explain how your child is doing by showing you examples of their work. The teacher may discuss your child's learning skills and work habits, and ways to support your child at home.</p> <p>The following provides strategies to help you make the most of the Parent-Teacher meetings:</p> <ul style="list-style-type: none">· Talk to your child before the meeting about what they like about school but also what they find difficult.· Think about the questions you want to ask the teacher before the meeting. It is good to keep notes of your questions.· Find out from the school if you can have an interpreter or staff member that speak your language or if you can get support from the YMCA School Settlement Make sure to arrive 5 minutes before your meeting. If further conversation is required with the teacher, arrange a date and time for follow up.· After the meeting, talk with your child about the positive things that were discussed, and any specific concerns that were raised. Explain any plans that have been arranged to address these concerns. <p>It is helpful to stay in touch with your teacher, even when things are going well. Possible questions you can ask at the Parent-Teacher meeting?</p> <ul style="list-style-type: none">· How is my child adjusting to school?	<p>Mikutano ya Wazazi na Walimu</p> <p>Kwa darasa la msingi hadi 12, mikutano ya Wazazi na Mwalimu hufanyika mara mbili kwa mwaka. Tarehe zinawekwa kwenye kalenda ya shule na mawasiliano yatatumwa kwa wazazi. Ili kuhudhuria, wazazi wanapaswa kujiandikisha mtandaoni ili kuweka miadi. Wazazi wanahimizwa kuhudhuria mkutano huo ambao ni kwa dakika 10-15.</p> <p>Mikutano ya wazazi na mwalimu ni mazungumzo kati ya mzazi na mwalimu kuhusu kile kilicho bora kwa mtoto. Ni fursa ya kujadili maendeleo ya mtoto wako. Mwalimu ataeleza jinsi mtoto wako anavyoendelea kwa kukuonyesha mifano ya kazi zake. Mwalimu anaweza kujadili ujuzi wa mtoto wako wa kujifunza na tabia za kazi, na njia za kumsaidia mtoto wako nyumbani.</p> <p>Yafuatayo hutoa mikakati ya kukusaidia kufanikisha mikutano ya Wazazi na Mwalimu:</p> <ul style="list-style-type: none">· Ongea na mtoto wako kabla ya mkutano kuhusu kile wanachopenda kuhusu shule lakini pia kile wanachokiona kuwa kigumu.· Fikiria kuhusu maswali unayotaka kumuuliza mwalimu kabla ya mkutano. Ni vizuri kuweka maelezo ya maswali yako.· Tafuta kutoka shuleni ikiwa unaweza kuwa na mkalimani au mfanyakazi anayezungumza lugha yako au ikiwa unaweza kupata msaada kutoka huduma za shuleni za YMCA. Hakikisha unafika dakika 5 kabla ya mkutano wako. Ikiwa mazungumzo zaidi yanahitajika na mwalimu, panga tarehe na muda wa kufuatilia.· Baada ya mkutano, zungumza na mtoto wako juu ya mambo mazuri yaliyojadiliwa, na kero zozote maalum ambazo ziliibuliwa. Eleza mipango yoyote ambayo imepangwa kushughulikia kero hizi. <p>Inasaidia kuwasiliana na mwalimu wako, hata wakati mambo yanakwenda vizuri. Maswali yanayoweza kuulizwa kwenye mkutano wa Wazazi na Mwalimu?</p> <ul style="list-style-type: none">· Mtoto wangu anazoeaje shule?
--	--

<ul style="list-style-type: none"> · How is my child progressing in (name the subject)? · What subjects is my child receiving more support in? · What kind of support is my child receiving? · How can I help my child at home? · How is my child with other students? <p>Please share information about your child as well, such as what they enjoy doing, what they are good at, and how they learn best.</p> <p>It is important for the teacher to know about your child so they can support them as best they can in the classroom.</p> <p>Parents/guardians can take their child to the Parent-Teacher meetings</p>	<ul style="list-style-type: none"> · Mtoto wangu anaendeleaje kwenye (jina la somo)? · Mtoto wangu anapata msaada zaidi kwenye somo lipi? · Mtoto wangu anapata msaada wa aina gani? · Ninawezaje kumsaidia mtoto wangu nyumbani? · Mtoto wangu yukoje kwa wanafunzi wengine? <p>Tafadhali shirikisha taarifa kuhusu mtoto wako pia, kama vile kile anachofurahia kufanya, kile anachofanya vizuri, na jinsi gani wanajifunza vizuri.</p> <p>Ni muhimu mwalimu kujua kuhusu mtoto wako ili aweze kumsaidia kadri anavyoweza darasani.</p> <p>Wazazi/walezi wanaweza kuja na mtoto wao kwenye mikutano ya Wazazi na Mwalimu</p>
---	---

